



AITEL END OF TERM 1 2024 ASSESSMENTS

S.3 KISWAHILI END OF TERM ONE 2024 ASSESSMENTS

MUDA:2:30HRS

MAAGIZO:JIBU MASWALI YOTE.

1. Andika barua ya kirafiki kwa mamako. Mwambie kuhusu masomo yako shuleni na umwombe aje kukuona kwenye siku ya kutembelea wanafunzi shuleni. Mwombe pia akuletelee vitu mbalimbali unavyotaka yaani chakula, matunda, soda, nanasi, maziwa nk.

2. soma na kukariri shairi lifuatalo na kisha ujibu maswali yafuatalo.

ULEMAVU SI UPUNGUFU

Nakiri ni hitilafu, tofauti kwa wengine,

Pengine ninalemewa, kutekeleza kinyie,

Mungu wako ndiye wangu, uhai twaenda sare,

Ulemavu si kikwazo, cha kutoshiriki kazi.

Elimu tuko pamoja, diguri sote twawinda,

Ubaguzi sitaraji, kwako wewe ndugu yangu,

Ushirikiano tele, faraja tupeaneni,

Ulemavu si kikwazo, cha kutoshiriki kazi.

Kazi nydingi twashiriki, biashara tuko sote,

Michezo na burudani, na za wasiosikia,

Olimpiki za kipeke, na za wasiosikia,

Ulemavu si kikwazo, cha kutoshiriki kazi.

Haki zetu zajulika, nchini na duniani,

Mabungeni twakilishwa, katika twaitetea,

Nchi sote twaijenga, ni Zaidi ya mmoja,

Ulemavu si kikwazo, cha kutoshiriki kazi.

Jibu maswali yafuatayo.

(i) Shairi hili linahusu nini?

(ii) Shairi hili lina beti ngapi?

(iii) Andika mstari unaojirudiarudia katika kila ubeti.

(iv) Andika kibwagizo cha shairi hili.

(v) Mshairi anahimiza nini katika ubeti wa pili? Fafanua katika lugha ya kawaida.

3. Jaza mapengo kwa kutumia maneno yanayofaa kutoka boksi ifuatayo.

Kunusa, Mungu, Miguu, Midomo, Kuandika, Moyo, Kusikia, ona, meno, pua.

.....aliumba binadamu. Alimpa.....ya kutembea.

Alimpa.....ambao ndio unafanya kama injini ya mwili. Ndiyo unaosukuma damu mwilini kote. Pia, alimpa masikio ambayo anayatumia..... Alimpa macho pia.

Haya anayatumia ku..... . Mimi, Mungu alinipa.....ambayo ninayatumia kutafuna chakula.

Pia alinipa pua. Pua yangu inanisaidia ku..... .

.....ndiyo inanisaidia kutambua kama kitu Fulani kinanuka au kinanukia. Halafu alinipa mikono. Ninatumia mikono yangu..... .

4.(a) Madawa ya kulevya ni nini?

(b) Orodhesha aina kumi(10) za madawa ya kulevya nchini Uganda.

(c) Eleza athari (5) za madawa ya kulevya katika jamii.

Jadili njia tano (5) zakuzuia athari za matumizi ya madawa ya kulevya.

- 5.(a) Majanga ni nini?
- (b) Orodhesha aina kumi(10) za majanga katika Afrika Mashariki.
- (c) Jadili njia mbali mbali za kuepukana na majanga katika Afrika Mashariki.
- (d) Jadili njia mbalimbali za kukomesha majanga katika nchini Uganda.

- 6.(a) Kwa ufupi, tambua msamiati angalau kumi inayohusiana na haki za kibinadamu.
- (b) Orodhesha mifano kumi za haki za kibinadamu katika nchini Uganda.

- 7.(a) Weka sentensi zifuatazo katika hali ya mazoea.
- (i) Mpishi anatupikia chakula shulenii.
- (ii) Majanga ya moto ilitokea sana jikoni, viwandani na shulenii.
- (iii) Ardhi iliporomoka sana mahali pa milimani.
- (iv) Kolera inatokea wakati wa mvua na mafuriko

(b) Kanusheni sentensi zifuatazo

- (i) Maporomoko ya ardhi hutokeaa sana maeneo ya kigezi na Bududa.
- (ii) Wahasiriwa wa majanga huteseka sana nchini.
- (iii) Waziri mkuu huwatembelea wahasiri wa majanga kila ikitokea.
- (iv) Daktari huwatibusi wagonjwa hospitalini.

(c) Soma na kuigiza tanakali za sauti kutoka boksi.

Ng'o ngó ngó, chumbwi, pu, zii, tik tok tik tok, pya, jii.

- (i) Mti umeanguka chini.....
- (ii) Kengele iligonga.....
- (iii) Embe lilitumbukia majani.....
- (iv) Mwizi alitulia tulii baada ya chifu kumzaba kofi shavuni.....
- (v) Wanafunzi wote wamenyamaza.....
- (vii) Mali yote imezama.....

Downloaded from www.mutoonline.com

MWISHO

Downloaded from www.mutoonline.com